



DeKalb County
School District

Itifaki za Kuvaa Barakoa

(Kuanzia Julai 12, 2021)

Wilaya (DCSD) ya Shule za Kaunti ya DeKalb imejitolea kutoa mazingira salama ya kusoma kwa wanafunzi na wafanyakazi. DCSD ina furaha kuwarudisha wanafunzi kwenye majengo yetu ili tuendelee na misheni yetu ya kutoa huduma sawa za elimu za kukidhi mahitaji ya wanafunzi.

Wilaya inaendelea kufuatilia mitindo katika visa vilivyoripotiwa, ikiwemo ongezeko lililoripotiwa hivi karibuni katika kuenea kwa Aina ya Delta kati ya watu wasiokuwa na chanjo. Kulingana na Shirika la Afya Duniani, Aina ya Delta imekuwa Aina kuu ya Virusi vya Korona.

Maelezo yafuatayo yaliyosashishwa yatatoa mwongozo wa kuhakikisha kurudi shuleni, ofisini na vituoni kwa usalama, kuanzia na mapendekezo ya kusaidia kupunguza kuenea kwa COVID-19 katika majengo yetu.

[Kituo cha Kudhibiti Magonjwa \(CDC\) inapendekeza shule kuendelea kutumia mikakati ya sasa ya kuzuia COVID-19 kwa mwaka wa masomo wa 2021-2022.](#)

Mikakati muhimu ya mapendekezo ya CDC ya uzuiaji ambayo ni muhimu kwa masomo ya ana kwa ana na katika kusaidia kuzuia maambukizi ya COVID-19 shuleni ni pamoja na:

1. Matumizi ya jumla na sahihi ya barakoa.
2. Kutokaribiana na watu kadri iwezekanavyo.
3. Kunawa mikono na kufuata taratibu za kuzuia maambukizi ya kupumua.
4. Kusafisha na kudumisha vituo visafi.
5. Utafutaji wa watu waliokaribiana kwa kuchanganya na kuwatenga na karantini.
6. Kuwa mwangalifu kwa dalili za COVID-19, hasa ikiwa umekuwa karibu na mtu ambaye ni mgonjwa. Ikiwa una dalili za COVID-19, unapaswa kupimwa, kukaa nyumbani, na mbali na wengine.
7. Kupata chanjo.

Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb itatekeleza yafuatayo:

- **Wanafunzi wote ni lazima wavae barakoa wakiwa kwenye mabasi ya shule.** Hitaji hili linalingana na mapendekezo ya CDC ya kwamba watu wote wanapaswa kuvaa barakoa wakati wanatumia usafiri wa umma.
- **Barakoa zinahitajika** kwa wanafunzi wanaoenda shule ya msingi kwa kuwa hakuna upatikanaji wa chanjo kwa kundi la umri huu. Shule zitatumia kanuni zinazofaa katika kafeteria na maeneo mengine ambayo inaweza kuwa vigumu kwa wanafunzi kuvaa barakoa.

- Barakoa **zinahitajika** kwa wanafunzi wa shule ya kati na ya upili na hata pia kwa wafanyakazi wote. Ilijapokuwa barakoa kwa wafanyakazi na wanafunzi waliopewa chanjo kamili (umri wa miaka 12 na zaidi) ni za hiari kulingana na mwongozo wa CDC, kwa sababu uangalifu, barakoa zitahitajika katika majengo yote.

Wilaya itapitia mbinu zinazofaa ili kuwatambua wanafunzi na wafanyakazi ambao wamechanjwa na itatathmini upya kuvaa barakoa kwa hiari. **Wazazi wanahimizwa kushauriana na mtoa huduma wao kwa chaguo bora za chanjo kwa familia zao.**

- Wafanyakazi au wanafunzi ambao wana dalili za COVID-19 wanapaswa kukaa nyumbani mbali na wengine na watafute huduma kutoka kwa watoa huduma wao wa afya.

- Kuvaa barakoa **kunahitajika** kwa Mipango ya Siku Iliyoongezwa ya Baada ya Shule (ASEDP) kwa shughuli zinazofanyika ndani ya majengo. Barakoa ni za **hiari** kwa shughuli zinazofanyika nje.

- Barakoa ni za **hiari** kwa shughuli za michzo ya riadha. Barakoa **zinahitajika** katika vyumba vya kubadilishia nguo, na vyumba vya mazoezi. Timu za wanariadha zinapaswa kufuata itifaki zote zilizowekwa na Shirika la Shule za Upili za Georgia za usalama katika matukio ya michezo.

- Barakoa **zinahitajika** kwa vilabu vyote ambavyo vinakutanika ndani ya majengo. Barakoa ni za **hiari** kwa shughuli zinazofanyika nje.

- Wafanyakazi wataendelea kutumia Itifaki ya Wilaya ya COVID-19 wakati wanaripoti visa vya maambukizi ya COVID-19.

Shule na majengo ya Wilaya zitaendelea kutumia mikakati yote ya kupunguza hatari. Wilaya itaendelea kufuatilia visa katika Kaunti na Wilaya na Wilaya itakuwa na haki ya kusasisha kanuni zake, ikiwemo mahitaji ya wafanyakazi na wanafunzi wote kuvaa barakoa.

Wilaya itaendelea kufanya kazi na washiriki wa jamii kushughulikia maombi ya chanjo, upimaji wa kawaida au wa watu kulingana na utafiti wa hivi karibuni, ushauri wa matibabu na kuenea kwa visa.

